

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

TUME YA UTUMISHI WA UMMA

Simu: +255 (738) 166 703;
Nukushi: +255 (022) 2460117
Barua pepe: secretary@psc.go.tz
Tovuti: www.psc.go.tz



6 Mtaa wa Albert Luthuli,
Kitalu Na.10,
S.L.P. 9143,
11406 DAR ES SALAAM

TAARIFA KWA UMMA

UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA MASUALA YA KIUTUMISHI

Tume ya Utumishi wa Umma inapenda kuwakumbusha Waajiri na Taasisi za Umma kuwa wanatakiwa kuwasilisha Taarifa za masuala ya kiutumishi kwa kila robo (miezi mitatu) ya mwaka wa fedha husika.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 10 (2) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya **298**, Tume imepewa Mamlaka ya kuwataka Waajiri na Taasisi mbalimbali katika Utumishi wa Umma kuwasilisha taarifa kuhusu uendeshaji wa masuala ya Rasilimali Watu. Taarifa hizi ni chanzo kimojawapo kinachotumika kuonesha hali ya Utumishi wa Umma Nchini.

Tathmini ya hali ya uwasilishaji wa taarifa kutoka kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 inaonesha kuwa uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa masuala ya kiutumishi si wa kuridhisha. Baadhi ya Taasisi zilizopaswa kuwasilisha taarifa Tume, hazikutekeleza takwa hilo la kisheria kwa kipindi hicho na nyingine ziliwasilisha baada ya muda kupita.

Tume inawakumbusha Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu kuwasilisha taarifa zao kwa wakati ikizingatiwa kuwa uwasilishaji wa taarifa za masuala ya kiutumishi si jambo la hiari, bali ni takwa la kisheria.

Imetolewa na:-

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Nyakimura M. Muhoji'.

Nyakimura M. Muhoji,
KATIBU
TUME YA UTUMISHI WA UMMA